



# do **1** thing

*Misheni ya Do 1 Thing ni kuwahimiza watu, familia, biashara na jamii kujiandaa kwa hatari zote na kuweza kukwepa msiba.*

**LENGO:** Kuwa na uwezo wa kuwasiliana na wajumbe wa familia wakati wa msiba.

## Mpango wa Mawasiliano wa Familia

Leo tuna njia zaidi za kuongea wenyewe kwa wenyewe. Tumezoea kuwasiliana kwa simu, tovuti, na barua pepe, lakini misiba inaweza kubadilisha mambo. Huenda vifaa hivi visipatikane. Minara ya simu za mkononi huenda zikajaa watu wakijaribu kuwafikia marafiki na familia. Kama umeme umepotea nyumbani mwako, simu zisizokuwa na waya, tovuti, na barua pepe hazitafanya kazi pia.

**Chagua moja kati ya mambo yafuatayo ya kufanya mwezi huu ili ujiandae vyema:**

**Kuwa na simu yenye waya na chaja ya simu ya simu yako ya mkononi tayari iwapo umeme utapotea.**

Simu zisizokuwa na waya hazitafanya kazi wakati wa msiba kwa sababu zinahitaji umeme zaidi kuliko zinazopata kutoka kwa jaki ya simu. Simu za zamani zenye waya inayounganishwa kwenye kifaa hadi kwenye kituo zitafanya kazi hata wakati hakuna umeme. Hakikisha una angalau simu moja yenye waya katika nyumba yako iwapo umeme utapotea.

Weka chaja ya gari ya simu yako ya mkononi katika gari lako. Kama umeme umepotea nyumbani mwako, bado unaweza kuchaji simu yako katika gari lako.

Kama huna simu yenye laini na unatumia simu ya mkononi kama simu yako ya nyumbani, kumbuka kwamba minara ya simu ya mkononi huenda imeshikamana na simu wakati wa dharura. Hata hivyo, ujumbe wa maandishi kutoka kwa simu ya mkononi huenda ukawasilii wakati simu haiwezi. Hakikisha kila mtu katika familia yako anajua jinsi ya kutuma na kupokea ujumbe wa maandishi.



*Kumbuka, usipige simu kamwe kwa 911 ili upate maelezo kuhusu kinachoendelea wakati wa dharura. Piga simu kwa 911 kama umeumia au unahitaji msaada tu.*

## **Kuza mpango wa jinsi familia yako itawasiliana wakati wa msiba.**

Kuza mpango ili uweze kuwasiliana na famili yako wakati wa msiba. Jumuisha namba za simu za wanafamilia wote na wale ambao wanaweza kukupa msaada wa ziada, kama vile watoa huduma. Jumuisha pia namba zote za simu za kazini, shuleni, na huduma ya watoto, kama ipo. Fomu inayoteshea kwenye mkoba ambayo unaweza kutumia kuandika maelezo haya inaweza kupatikana katika [www.ready.gov](http://www.ready.gov). Hakikisha kila mmoja wa familia ana nakala ya mpango wako wa mawasiliano. Chapisha mpango wa mawasiliano kwa simu nyumbani mwako, na ujumuishe katika mfumo wako wa kubeba pia.

### Mwasiliani wa Nje ya Eneo

Simu za nchini na simu za mbali hufanya kazi katika mizunguko tofauti. Wakati mizunguko ya nchini imejaa kupita kiasi, huenda bado ukaweza kupiga simu za mbali. Chagua mtu nje ya eneo la upigaji simu la nchini awe mwasiliani wako wa "nje ya Eneo". Hakikisha wanafamilia wote wanabeba namba hii ya simu. Kitu kikifanyika wakati familia yako haiko pamoja na hamwezi kuwasiliana, kila mmoja wa familia anaweza kupigia simu mwasiliani wa "nje ya eneo" na kuwacha ujumbe kwa ajili ya wengine.



### **Salama na Mzima**

Mpango wa Msalaba Mwekundu wa Salama na Mzima ni njia ya familia kuwasiliana wakati wametenganishwa wakati wa msiba. Tembelea sasa wavuti katika [www.safeandwell.org](http://www.safeandwell.org) na uwaonyeshe wanafamilia jinsi inavyofanya kazi.

Fanya anwani ya wavuti sehemu ya maelezo ya dharura ambayo kila mwanafamilia anabeba. Kama mmetenganishwa wakati wa msiba, hakikisha kila mtu anajua kwenda kwenye wavuti ili kuingiza maelezo kujihusu, na jinsi ya kupata maelezo juu ya wengine.

## **Panga namba za Wakati wa Dharura (ICE) katika simu za mkononi za familia yote.**

Kama umeumia na huwezi kuongea, watu wa kwanza wanaoitikia na wafanyi kazi wa hospitali huenda wasijue jinsi ya kuwasiliana na familia yako moja kwa moja. Kama una simu ya mkononi, unaweza kuwapa namba za simu za waasiliani wako wa dharura kwa watu wanaoitikia kwanza na wafanyi kazi wa hospitali.

1. Unda mwasiliani mpya katika kitabu chako simu ya mkononi.
2. Mpe jina mwasiliani wa ICE.
3. Ingiza namba zote za simu za mtu ambaye ungependa afahamishwe wakati wa dharura ya matibabu.